

## MKATABA WA UPANGAJI

Mkataba huu umeandikwa tarehe .....<sup>1</sup>.....mwezi.....**Januari**..... mwaka .....**2024**.....

Kati ya

**HADIJA ALLY ELMI** Mtanzania Mkazi wa Arusha na mmliki wa nyumba iliyopo kata ya Leveolosi mkoa na wilaya ya Arusha katika mkataba huu atatambulika kama “**Mwenye Nyumba**”

Na

**THOMAS SAVUTU MSOFE T/A SAVUTU HARDWARE** Mtanzania, mfanya biashara wa **S.L.P 7284** Arusha, ambaye katika Mkataba huu atatambulika kama “**Mpangaji**”

**WAKATI AMBAPO**, Mwenye Nyumba na Mpangaji wamekubaliana yafuatayo katika mkataba huu:-

1. Kwamba, Mwenye Nyumba na Mpangaji wamekubaliana kuwa Mwenye Nyumba atampangishia Mpangaji nyumba matumizi ya ofisi za vifaa (Hardware) katika nyumba yake iliyopo Kata ya Levolosi naye Mpangaji ameridhia kupanga nyumba hio.
2. Kwamba, Mwenye Nyumba na Mpangaji wamekubaliana kuwa kodi ya pango ni kiasi cha shilingi milioni moja na laki nane na elfu hamsini tu (1,850,000/-) kwa mwezi mmoja.
3. Kwamba pande zote mbili zimekubaliana kuwa mkataba huu utadumu kwa muda wa miezi thelathini na sita (**36**) kuanzia tarehe 1 Mwezi Januari 2024 mpaka 31 Disemba 2026. Ambapo malipo yaliyotajwa katika aya ya pili ya mkataba huu yatalipwa kwa awamu ambapo Mpangaji atalipa kiasi cha milioni moja na laki nane na elfu hasmini (1,850,000/-) kila baada ya miezi kumi na mbili.
4. Kwamba, pande zote mbili zimekubaliana kuwa, malipo katika aya ya pili ya mkataba huu yatalipwa mwanzoni mwa kipindi husika cha mkataba tu na sio mwishoni. Endapo Mpangaji atakatisha mkataba huu kabla ya kipindi chake kuisha Mpangaji hata kuwa na haki ya kumdai Mwenye Nyumba amfidie kwa kipindi ambacho Mpangaji atakuwa amelipia.

5. Kwamba, Mwenye Nyumba na Mpangaji wamekubaliana kuwa upangaji huu hautarithishwa kutoka kwa Mpangaji kwenda kwa mtu mwingine wala Mpangaji haruhusiwi kumpangishia mtu mwingine (Sub-Lease).
6. Kwamba, Mwenye Nyumba na Mpangaji wamekubaliana kuwa Mpangaji atalipa malipo ya umeme, maji kila mwezi pamoja na usafi wa nyumba, malipo ya taka na mazingira yote yanayozunguka nyumba aliyopanga na malipo haya ni tofauti na kodi ya upangaji wa nyumba uliotajwa katika aya ya pili ya mkataba huu.
7. Kwamba, Mwenye Nyumba na Mpangaji wamekubaliana kuwa Mpangaji kutumia nyumba aliyopangishwa pekee yake kwa matumizi yaliyoainishwa kaika mkataba huu na sio kwa ajili ya shughuli nyingine yoyote.
8. Kwamba pande zote mbili zimekubaliana kuwa endapo Mpangaji atakiuka sheria za nchi Mwenye Nyumba hatahusika kwa sheria yoyote itakayo mkingamia.
9. Kwamba Pande zote mbili zimekubaliana kuwa kushindwa kutumiza masharti ya mkataba huu ni kushindwa kuendelea na mkataba huu na endapo upande wowote utavunja masharti ya mkataba huu upande ulioathirika utakuwa huru kupuleka malalamiko katika vyombo husika.

Mkataba huu umesainiwa hapa Arusha tarehe .....<sup>1</sup>.....mwezi wa JANUARI mwaka .....  
2024

Mkataba huu umesainiwa Arusha na  
HADIJA ALLY ELMU anayetambulika  
Kwangu tarehe.....<sup>1</sup>.....mwezi JANUARI 2024

}



.....  
Mwenye Nyumba

**SHAHIDI WA MWENYE NYUMBA**  
ZUHURA THANO


Jina: .....

0652026474

Anuani/Simu : .....

Saini: .....  


Mkataba huu umesainiwa na  
**THOMAS SAVUTU MSOFE**  
ambaye anatambulika kwangu  
tarehe .....<sup>1</sup>.....mwezi JANUARI 2024



  
.....  
**Mpangaji**

**SHAHIDI WA MPANGAJI**

Jina: ..... LUCY FRANK .....


Anuani/Simu : ..... 0767255954 .....

Saini: .....  .....

**SAINI ZIMEWEKWA MBELE YANGU:-**

Jina: ..... MARIAM SAAD .....

Cheo: ..... WAKILI .....

Saini na Mhuri : .....  .....

Tarehe: ..... 2 - JANUARI -2024 .....

